# Kutoka Futuhi hadi Ufutuhi: Chimbuko, Maendeleo na Nadharia zake

**Athumani S. Ponera**

**Ikisiri**

*Makala haya yanaijadili dhana ya ufutuhi ambayo bado haijazoeleka kimatumizi katika fasihi ya Kiswahili. Makala yanajikita katika kujadili jinsi ufutuhi ulivyochimbuka kutoka katika dhana-mama ya futuhi, na kupata mwelekeo mpya wa kimatumizi. Ufafanuzi unaanzia kwenye mgongano wa kiistilahi kuhusu dhana kadhaa zinazotumiwa kumaanisha vipengele na matokeo ya ufutuhi. Kisha, umefuatia ufafanuzi unaoangazia maendeleo ya dhana ya ufutuhi kutokea kwenye fikra za futuhi; mwisho kuna maelezo ya kinadharia kuhusu utokeaji wake. Nadharia zilizojadiliwa ni tatu; nazo ni Nadharia ya Mkwezo, Nadharia ya Msigano, na Nadharia ya Burudiko. Mjadala umefanywa kwa shabaha ya kuijengea uhalali dhana hii mpya na jumuifu ili kupunguza matatizo ya mwingiliano na uradidi unaojidhihirisha katika kuzitumia dhana kama vile kejeli, dhihaka, tashtiti, utani, ucheshi, kicheko, na furaha ambazo zinaendana na ufutuhi.*

## 1.0 Utangulizi

### 1.1

Sehemu hii inajadili dhana ya ufutuhi na nyinginezo zinazoizungukia kama zilivyododoswa katika ikisiri. Mjadala unagusia maana ya ufutuhi, mwingiliano wa kiistilahi kuhusu vijenzi vyake pamoja na mwingiliano wa kiistilahi kuhusu matokeo ya vijenzi hivyo. Mwisho limetolewa hitimisho kuhusu mwingiliano huo.

Dhana ya futuhi imekuwa ikitumiwa kwa muda mrefu katika taaluma za fasihi ya Kiswahili. Dhana nyingine ambazo zinaizungukia dhana hii kimaana ni kama vile ucheshi, kicheko, furaha, raha, kejeli, dhihaka, na ubeuzi. Aghalabu, mijadala mingi kuhusu dhana hizi imekuwa ikitoa mahitimisho yanayoelekeana na kuingiliana, hasa katika vipengele vya vijenzi na matokeo yake (kwa mfano, tazama Sengo na Lucas, 1975; Beck, 1999; Provine, 2000; Dauphin, 2007 na Mrikaria, 2010). Ili kupunguza hali hiyo ya mwingiliano, ndipo mwandishi wa makala haya anapoiibua dhana ya ufutuhi.

### 1.2 Dhana ya Ufutuhi

Dhana ya ufutuhi inatumiwa kama kisawe cha neno la Kiingereza '*comic*' ambalo ni nomino inayodokeza hali. Ufutuhi unajadiliwa kama hali ijengwayo na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto hadi kuwafanya watu wachangamke, wafurahi, na watabasamu au wacheke. Fasili hii inatumulikia ukweli kuwa ufutuhi hujumuisha mambo matatu kwa pamoja; mambo hayo ni ucheshi, vicheko, na furaha. Kimsingi, dhana hii ya ufutuhi imepatikana kutokana na upanuzi wa maana-msingi ya dhana ya futuhi; yaani, kijitapo cha tamthiliya ambacho hutawaliwa na u-nyemi. Kwa hiyo, ufutuhi ni dhana inayoweza

kujidhihirisha hata katika tanzu za fasihi zilizo nje ya utanzu wa tamthiliya kama vile ushairi, nathari pamoja na Fasihi Nenwa[1]. Dhana ya ufutuhi imetofautishwa na ile ya futuhi kwa msingi wa kwamba, futuhi, kwa kiasi kikubwa, hujiegemeza zaidi katika suala la utendaji, hususan matendo ya jukwaani; ilhali, ufutuhi huvuka mipaka ya jukwaa na kuchupa hadi katika mazingira mengine ya kimaisha kama vile katika uendeshaji wa shughuli za kiuchumi (kwa mfano, shambani, sokoni, dikoni, au bandarini), katika uandishi wa bunilizi mbalimbali, pamoja na kwenye mawasiliano ya kawaida wafanyianayo watu katika maisha yao ya kila siku.

Masuala yanayohusiana na ufutuhi yamekuwa yakifafanuliwa toka miongo mingi iliyopita kupitia taaluma ya Jelotolojia. Kwa mujibu wa Fry (1963; 1976; 1998; na 2000), Jelotolojia ni taaluma inayochanganua maana, aina, utokeaji, historia, mawanda, upokezi pamoja na athari za ucheshi, furaha, kicheko na michakato yoyote ya ki-futuhi. Kietimolojia, dhana ya Jelotolojia imejengwa na mizizi miwili ya lugha ya Kiyunani; wa kwanza ni *gelos* wenye maana ya kicheko, na wa pili ni *ology* unaomaanisha taaluma. Usuli wa kuibuka kwa dhana hii unanasibishwa sana na taaluma za Saikolojia (taaluma ihusuyo uchanganuzi wa akili ya mnyama) na Fiziolojia (kijitawi cha Biolojia kinachochanganua mifumo mbalimbali ya viumbe hai na jinsi inavyotenda kazi). Mtazamo huo wa awali uliyatazama masuala yabebwayo na taaluma ya Jelotolojia kama nyenzo ya kitabibu kwa wagonjwa waliokuwa na matatizo ya kiakili. Mwasisi wa taaluma ya Jelotolojia ni William Fry[2]. Mwanzoni, aliihusisha zaidi na taaluma za kitabibu; na baadaye, akichagizwa na mawazo ya wataalamu wengine kama vile Robert Provine, akapanua wigo wa kifikra na kuihusisha na fani za sayansi za jamii (Provine, 2000; na Schuette, 2010).

Baada ya kushughulikiwa kwa muda mrefu ikiegemezwa katika taaluma hizo, baadaye, Jelotolojia ikaanza kuchimbuliwa ikihusishwa na mitalaa ya sayansi za jamii, ikiwamo sanaa. Kwa upande huu wa fani za sayansi za jamii, kwanza iliegemezwa katika sanaa ya uchoraji pekee, baadaye ikaingizwa katika fasihi. Taaluma hii ilichukua mwelekeo mpya wa kiistilahi katika sayansi za jamii pamoja na ukweli kuwa iliendelea kushughulikia nguzo-msingi zilezile (k.v. maana, aina, utokeaji, historia, mawanda, upokezi na athari za ucheshi, furaha, na kicheko). Istilahi iliyoonekana kuwa na mashiko huku ni ufutuhi (*comic*) kuliko ile ya Jelotolojia.

---

[1] Dhana hii inatumiwa kama kisawe cha dhana ya *Oral Literature*; kwa maana ya fasihi itolewayo kwa uneni (ambapo usimulizi hujitokeza kama dhana bebwa tu ya uneni). Hii ni istilahi inayoonekana kuwa na mashiko kuliko ile ya Fasihi Simulizi ambayo imezoeleka. Istilahi ya Fasihi Nenwa ina uwezo wa kuzijumuisha dhana zote zitolewazo kwa uneni na matendo au ishara zikiwamo semi ambazo, kwa hakika, kimantiki si sahihi kujumuishwa katika dhana ya usimulizi.

[2] Huyu ni Mmarekani aliyezaliwa Machi 25, 1924 huko Cincinnati, Ohio. Kwa zaidi ya miaka 30 ameifanyia kazi taaluma ya Jelotolojia. Ndiye anayetajwa kama 'baba wa Jelotolojia'.

Dhana hii ya ufutuhi huleta mikanganyiko miongoni mwa watumiaji wa lugha. Mkanganyiko huo hutokea katika kufafanua dhana mbalimbali zenye uwezo wa kuzaa ufutuhi kama vile kejeli, kijembe, tashtiti, stihizai, dhihaka, kinaya, ubeuzi, utani, pamoja na ufyosi. Mkanganyiko huo huwa mkubwa zaidi pale dhana hizo zinapohusishwa na matokeo yanayotokana nazo. Matokeo hayo ni uchangamfu, furaha, tabasamu au kicheko. Matokeo hayo huchukuliwa kuwa ni ufutuhi. Hata hivyo, licha ya mtazamo huo wa kwanza wa ufutuhi (wa kujiegemeza kwenye matokeo ya vijenzi), mtazamo wa pili ni mpana zaidi. Kwa upeo huo mpana, ufutuhi huchukuliwa kuwa ni mchakato; yaani, ni jumla ya vitu vyote vinavyounda mazingira ya kutokea kwa tabasamu, kicheko, au furaha. Vitu hivyo hujumuisha mhusika mwenyewe, maneno au matendo yake, hatua za utendaji au unenaji, pamoja na mwonekano wake.

## 1.3 Mgongano wa Kiistilahi kuhusu Vijenzi vya Dhana ya Ufutuhi

### 1.3.1 Futuhi

Kisawe cha futuhi kwa lugha ya Kiingereza ni '*Comedy*.' Neno hili linatokana na neno *Komos* la lugha ya Kiyunani linalomaanisha sherehe za matambiko ya jamii za watu wa Uyunani ya Kale. Katika sherehe hizo watu walifurahi kwa kuimba, kucheza ngoma na kutamba majigambo ili kumshukuru mungu wao aitwaye Dionysius ambaye ni mungu wa rutuba na mavuno (Encarta, 2007; Kennedy na Gioia, 2007: 1257). Kwa hiyo, kwa jicho la kitaaluma, futuhi ni utanzu wa kidrama ambao shabaha yake kuu ni kufurahisha. Miongoni mwa sifa za msingi za utanzu huu ni ile ya utunzi na utendaji wake kuelekezwa na utendekaji wa jukwaani au mbele ya hadhira.

Kennedy na Gioia (2007) wanafafanua kuwa futuhi za mwanzo kabisa zilizokuwa katika umbo lililoandikwa zilipatikana huko Uyunani katika mji wa Athens mnamo karne ya 5 Kabla ya Kristo (KK). Futuhi hizo zilikuwa za Aristophanes (448-385 KK) ambaye aliziunda kwa kutumia kejeli; zilikuwa zinazungumzia masuala ya siasa za Athens, falsafa, pamoja na sanaa ya wakati huo. Katika zama hizo pia kulikuwa na futuhi zilizotungwa na Menander (342-291KK)[3] ambaye alikuwa anatoa changamoto kwa Aristophanes. Futuhi za wakati huo zilikuwa zinatendeka nyakati za mchana katika kipindi cha sherehe za msimu wa baridi. Wakati futuhi za Aristophanes zilijikita katika uhalisi, zile za Menander zilikuwa kinyume chake (zilitumia mandhari na wahusika wa kubuni).

---

[3] Menander (342 - 291 KK), ni mwandishi maarufu wa kazi za futuhi kutoka Uyunani. Ni miongoni mwa waandishi walioandika futuhi katika kipindi kilichojulikana kama 'Kipindi cha Futuhi Mpya'. Menander aliandika zaidi ya kazi 100 za futuhi. Kazi zake ziliendelea kuigizwa kwa kipindi kirefu baada ya kifo chake. Baadhi ya kazi zake maarufu ni *The Arbitration, The Rape of the Ringlets, Samia,* na *The Curmudgeon* (*Encarta Encyclopedia*, 2007).

Green (1977) na Olson (2007) wanaongezea kuwa futuhi zilikuwa zinafanyika jukwaani huko Syracuse katika jiji la Sicily, Uyunani, kuanzia katikati ya miaka ya 480. Huko Athens, katika miaka hiyohiyo, mashindano ya ushairi wa kifutuhi yaliongezwa katika programu rasmi za kisanaa katika jiji la Dionysia mnamo mwaka 486; na takriban miongo minne baadaye, hatua kama hiyo iliafikiwa katika jiji la Lenaia. Maelezo haya ya Green na Olson yanawiana na yale ya Aristotle katika *The Poetics* (uk. 2), anaposema kuwa chimbuko la futuhi limo katika masuala ya 'ushairi uliopindishwa'. Hata hivyo, Aristotle anaongezea kuwa futuhi haukuwa utanzu uliopewa kipaumbele kama ilivyokuwa kwa tanzia. Hii yatokana na ukweli kwamba wakati wa zama za Plato, Aristotle, na Socrates, utanzu huu ulikuwa ni wa kitabaka. Kuanzia muda huo, usanaji na utendekaji wa futuhi ulienea katika jamii mbalimbali barani Ulaya na duniani kwa jumla. Matukio hayo yote yaliambatana na ucheshi au furaha iliyotokana na majigambo na tambo zilizokuwa na dhihaka na utani ndani yake. Baadaye, matukio hayo yaliingizwa katika kazi mbalimbali za fasihi andishi kama vile nathari, tamthiliya na ushairi.

### 1.2.2 Kejeli

Msokile (1992: 51) anaifasili dhana hii kwa kusema: "Kejeli au kinaya au stihizai hukusudia kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa au kinyume na ukweli ulivyo." Naye, Wamitila (2003a: 79), kwa upande wake, anaielezea kejeli au kinaya kuwa ni hali yoyote inayodokeza unyume katika tukio, usemi au hali. Wamitila anasonga mbele zaidi kwa kuonesha mgawanyo wa kejeli; ambapo, anatubainishia kuwapo kwa kejeli ya hali, kejeli ya balagha, kejeli ya kidrama, kejeli ya kiusemi (ya kitoni), na kejeli ya kijaala. Aidha, kwa mujibu wa *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010: 150), kejeli ni neno au tendo la kuonesha dharau kwa mtu. Kwa jumla, kejeli ni hali, maneno au matendo yenye unyume ndani yake. Istilahi nyingine yenye maana sawa na kejeli ni kinaya. Unyume huo hufanywa kwa lengo la kudharau, au kuonesha mzaha. Lengo la kejeli ni kushambulia, kuchekesha au kuadilisha. Kejeli inayoshambulia bila kuchekesha ni masimango. Kwa hiyo, kwa kawaida, kejeli huambatana na hali ya furaha au kicheko. Kijenzi hiki cha ufutuhi hujitokeza sana katika lugha ya mazungumzo ambayo watu huitumia kila siku. Jambo la muhimu katika maelezo haya ni ukweli kuwa, kejeli, kwa namna moja au nyingine, huhusisha ubezaji, balagha, utani, dharau, na unyume wa mambo. Hata hivyo, dhana ya unyume wa mambo ndiyo kiini cha kejeli. Zaidi, ni ukweli kuwa upande wa pili wa kejeli (tukiacha ule wa kufanyiwa unyume—kukejeliwa), huhusisha ucheshi, furaha, na kicheko (dhana hizi tatu zimefafanuliwa katika sehemu ya 1.3 ya makala haya).

### 1.2.3 Ubeuzi

Kwa mujibu wa Mohamed na Mohamed (2004), neno ubeuzi linatokana na kitenzi 'beua' au 'beza' chenye maana ya tweza, dharau, bekua au puuza. *Kamusi ya*

*Kiswahili Sanifu* (2004) inafafanua zaidi kwa kusema kuwa utwezaji, dharau, udunishaji au upuuzaji huo hufanywa kwa maneno au matendo. Kezilahabi (1976: 82) anaongezea kuwa maneno au matendo ya kibeuzi hufanywa kwa kunyunyiziwa utani na dhihaka kwa lengo la kudhihaki na kushusha hadhi ya mtu. Anaendelea kwamba, ubeuzi hutumia maneno ambayo humhitaji mtu afikiri kwa kina ili kutambua ujumbe uliomo. Wakati mwingine ubeuzi hutumia mafumbo ingawa siyo mazito kama yatumiwavyo katika vijembe. Kutokana na fasili zilizotolewa na wataalamu hao, inaonekana tena hapa kuwa ubeuzi unahusiana kwa namna moja au nyingine na ufumbaji, na unyume. Zaidi ya hayo, maneno na matendo hayo ya kibeuzi aghalabu huweza kuzua hali ya furaha, au kicheko au ucheshi kwa watazamanji au wasikilizaji.

### 1.2.4 Kijembe

Vijembe ni maneno au utungo wa mafumbo au wa mzunguko wenye kumsema mtu kwa mabaya. Aghalabu, mtoa kijembe hufanya hivyo kwa lengo la kujikweza, huku akimtweza mpigwa kijembe (Msokile, 1992; Wamitila, 2003b; na Mohamed na Mohamed, 2004). Msingi mkubwa wa vijembe ni mafumbo. Mara nyingi, mafumbo hayo huweza kueleweka kwa anayefumbiwa pamoja na wafuatiliaji. Hata hivyo, mfumbiwa hukosa uwezo wa kumjibu au kumshambulia mpiga kijembe kwa kuwa hukosa ushahidi wa wazi kuhusu uhusika wake katika kijembe hicho. Aghalabu, ufundi huo wa kufumba na kuyazungusha maneno, hufanywa katika namna ambayo husababisha hali ya kufurahi kwa wanaosikiliza, siyo kwa apigwaye vijembe.

### 1.2.5 Tashtiti

Kwa mujibu wa Wamitila (2003a: 223), tashtiti ni mbinu ya utunzi wa kazi ya sanaa ambapo mtunzi hutumia vichekesho, kinaya, kijembe, ubezaji, na dhihaka katika kufichua maovu ambayo yamesakini na kutawala katika jamii. Kutokana na mawazo ya jumla ya Wamitila, tashtiti yaonekana kuwa ni sanaa ya matumizi ya maneno yaliyoteuliwa na kupangiliwa vyema. Shabaha yake kuu ni kumtweza mtu, tabaka, au jamii fulani. Kwa upande mwingine, matumizi ya tashtiti husababisha kicheko, furaha au ucheshi kwa wafuatiliaji. Hivyo basi, tashtiti yaweza kutazamwa kwa kuhusishwa na sifa zifuatazo: mosi, hujitokeza katika matini kwa namna ya ujumla (siyo lazima iwe katika umbo au ngazi ya neno, au tungo pekee). Pili, huweza kutumika kama mbinu ya kisanaa. Hii ni kutokana na ujumla huo uliotajwa katika hoja iliyoitangulia. Tatu, ni sanaa jumuifu; yaani, hubeba kwa pamoja kejeli (kinaya), kijembe, ubezaji, na dhihaka. Kwa mara nyingine, pamoja na maelezo haya kutuelekeza katika umahususi wa dhana ya tashtiti, bado yanatumulikia kuhusu kuwapo kwa mwingiliano baina yake na

vijenzi vilivyokwishafafanuliwa. Tashtiti huweza kubeba baadhi ya vijenzi kama vile kejeli na vijembe.

### 1.2.6 Ufyosi

TUKI (2004: 425) inafasili dhana hii inayotokana na kitenzi 'fyosa' kuwa ni tabia ya kutoa maneno ya utani au matusi lakini yasiyoleta ugomvi. Ihusishwapo na ufutuhi, mshindilio wa maana ya dhana hii unawekwa kwenye hali ya utumiaji wa matusi. Hiki ni kipengele muhimu katika uhusiano wa kiutani; ambapo, watanianao huweza kufanya mawasiliano (ya kuhabarishana, kuonyana, au kuelimishana) kwa kutumia lugha yenye matusi.

### 1.2.7 Stihizai

Stihizai, kwa mujibu wa TUKI (2004: 383), ni maneno anayoambiwa mtu kwa utani kwa madhumuni ya kumdharau au kumkejeli. Fasili ya Wamitila (2003a: 204-205) inapiga hatua ya mbele zaidi kwa kueleza kuwa stihizai hutumiwa kuelezea shambulio la kiucheshi lenye nia mbaya ya kiwivu ambalo humkusudia mtu. Mwingiliano wa dhana hii na ile ya tashtiti unadhihirika kupitia ukweli kuwa stihizai ni sehemu tu ya tashtiti; kwamba, hujipambanua kwa kutumia sanaa ya kitashtiti. Tofauti baina yake iko kwenye dhana ya kumwonea mtu wivu au kijicho kama ambavyo imedokezwa.

### 1.2.8 Utani

Wamitila (2003a: 331) anaifasili dhana hii kuwa ni "...hali ya kufanyiana mizaha miongoni mwa wanajamii au jamii mbalimbali bila ya kuogopa wala kushtakiana." Akiendelea kueleza kuhusu shabaha ya utani ambao anauita kuwa ni desturi ya jadi kwa makabila mengi, anasema "...ni kupunguza uhasama au chuki baina ya makundi ya watu." Maneno au matendo yahusuyo utani huwa na umbo na sifa zake maalumu. Kwa mujibu wa Aldama (2009) na Attardo (2001), utani huwa na sifa zifuatazo: (a) hufanyiwa mazoezi na mnenaji au mtendaji kabla ya kuudhihirisha; (b) mdhihiriko wake hutegemea sana muktadha; (c) huwa huru kuundwa na yeyote; (d) muundo-msingi wake ni uleule; ila hubadilishwa na mnenaji au mtendaji kulingana na mabadiliko ya muktadha; na (e) huwa na mwingiliano wa vipengele vihusikavyo katika kuutengeneza. Vipengele vinavyokusudiwa hapa ni kama vile kejeli, vijembe, dhihaka, na ufyosi. Hivyo, waandishi au watenzi wake hutumia mseto wa vipengele hivyo.

Kwa jumla, kiini cha utani kimo katika uhusiano wa kijamii unaoruhusu watu kutoleana maneno au kufanyiana matendo yenye dhihaka, vijembe na kejeli; aghalabu, kwa lengo la kuonya, kufurahisha na kuchekesha. Utani unaweza kujitokeza katika umbo la nyimbo, matendo, mazungumzo marefu au kauli fupifupi. Hiki ni kipengele maarufu sana katika maisha ya jamii nyingi za hapa Tanzania. Umaarufu na kuzoeleka kwake husababisha kionekane kama ni kipengele cha lazima katika maisha ya jamii hizo. Akiyakinisha kuhusu kushamiri

kwa utani, Mulokozi (1986: 668), anasema kuwa utani (kwa lugha ya Kihaya ni '*kusilibya*') ni sanaa ambayo imeenea katika jamii ya Buhaya na katika jamii nyingine nyingi za Kiafrika huku suala hilo likitawaliwa na kanuni mbalimbali. Jambo la ziada linaloweza kupatikana kutoka katika uyakinishaji huu wa Mulokozi ni jinsi anavyoubainisha utani kwa jicho la kisanaa.

Katika jamii nyingi za Tanzania, utani hujidhihirisha katika aina zifuatazo: utani wa kabila na kabila, wa marafiki, wa wanarika, pamoja na wa kifamilia (mjomba na wapwawe, mashemeji, pamoja na ule wa babu au bibi na wajukuu wake). Makundi yote ya watani kutoka katika aina hizo huwa huru kutumia vipengele mbalimbali vya kauli kama vile methali, vitendawili, nahau, simo na simulizi fupi wakati wa kutaniana. Aidha, kwa kawaida, utani wowote lazima uwe umejikita katika miktadha mbalimbali ya kimaisha inayowazunguka wale wanaotaniana. Ni vigumu kwa watu ambao hawajuani kwa undani kutaniana (Sengo na Lucas, 1975: 51-57). Kati ya aina hizo za utani, aina inayotamalaki sana katika jamii ni ile inayohusisha kabila moja na jingine (Yahya-Othman na wenzake [h.t.]; Sengo na Lucas, 1975).

## 1.3 Mgongano wa Kiistilahi kuhusu Matokeo ya Vijenzi vya Ufutuhi

### 1.3.1 Ucheshi

Kwa mujibu wa TUKI (2004: 14), ucheshi ni hali ya kuwa mchangamfu na mwenye furaha kwa mtu au watu wengine. Katika maisha ya kawaida (yaani, nje ya fasihi) dhana hii huhusishwa na tabia; aghalabu, tabia ambayo mtu huidhihirisha kwa muda mrefu, pengine huzaliwa nayo. Hivyo, isemwapo, mathalani, 'Athumani ni mcheshi', maana ya jumla na ya haraka inayopatikana hapa ni ile inayohusisha mwonekano wa kawaida wa Athumani, na siyo hali aliyoionesha kwa siku moja. Kifasihi, ucheshi huchukuliwa kuwa ni mbinu mojawapo ya kuundia tashtiti. Maelezo haya yanatupatia hoja muhimu kuwa ucheshi hujumuisha uchangamfu, ukunjufu wa moyo, pamoja na furaha.

### 1.3.2 Furaha

Furaha ni kionjo cha kisaikolojia kinachohusu hali ya ukunjufu wa moyo na bashasha ambayo aghalabu, hutokana na ridhiko la moyo (au nafsi). Ridhiko hilo la moyo na akili kama kiunzi muhimu cha kuwapo kwa furaha, mara nyingi, husababishwa na mtu kutenda au kutendewa matendo, kuambiwa maneno, au kutokewa na hali ambayo inaendana na matakwa, malengo, au vionjo vyake. Kionjo hiki huwa tofauti kati ya mtu na mtu au kati ya mazingira ya aina moja na nyingine. Mtu huweza kuwa na furaha bila kucheka, na mwingine huweza kucheka hata kama hana furaha. Kuna namna mbalimbali ambazo binadamu huzitumia kudhihirisha furaha; nazo ni kama vile miguno, mbinja, vicheko, vigelegele, vilio, mayowe, na kurukaruka.

Msingi wa tofauti kati ya furaha na ucheshi uko katika dhana ya tabia; yaani, furaha yaweza kuwa ni jambo linaloonekana kwa mtu katika baadhi tu ya nyakati au siku; ilhali, ucheshi waweza kuonekana katika sehemu kubwa ya maisha ya mtu (isipokuwa katika baadhi tu ya nyakati awapo katika miktadha ya majonzi kama vile msibani).

### 1.3.3 Kicheko

Whipple na Calvert (2008) wanaifasili dhana ya kicheko kuwa ni mwitikio wa kibiolojia ambao mwanadamu huutoa kama kielelezo cha furaha. Kicheko ni sauti itolewayo na mtu achekapo; ambapo, huweza kumaanisha hali mbalimbali kama vile furaha, dharau (kubeua), au hata jitimai. Maelezo haya yanatuangazia kuwa kuna kicheko cha kuafiki, cha kukanusha, cha kubeza au kukejeli, cha kujengea au kukazia hoja, pamoja na cha kung'ong'a. Licha ya Whipple na Calvert kuielekeza zaidi fasili yao kwa mwanadamu, wanaendelea kufafanua kuwa kicheko huweza kutokea pia kwa wanyama wengine kama vile sokwe.

Whipple na Calvert (wameshatajwa) wanaendelea kueleza kuwa utokeaji wa kicheko hutofautiana kulingana na vigezo vya umri, jinsi, na kuwa au kutokuwapo karibu na aina fulani ya watu. Katika suala la umri, wanaeleza kuwa watoto hucheka mara nyingi zaidi (ambapo huweza kucheka hadi mara 300 kwa siku) kuliko watu wazima (ambao kiwango chao cha juu cha kucheka ni mara 17 tu kwa siku). Licha ya kwamba data hii inayowasilishwa na Whipple na Calvert inatokana na tafiti zilizofanywa nje ya bara la Afrika, ukweli kuhusu kuwapo kwa tofauti ya kiasi cha kucheka baina ya watoto na watu wazima unabakia hivyohivyo katika jamii zote. Kuhusu kigezo cha jinsi, wanaendelea kufafanua kuwa, kwa kawaida, sehemu kubwa ya wanaume 'huchekea ndani', yaani, hucheka kwa kujificha zaidi; ilhali, sehemu kubwa ya wanawake 'huchekea nje', yaani, hucheka bila kujificha. Zaidi, tunafafanuliwa na wataalamu hawa kwamba mwanadamu hucheka zaidi awapo mbele ya mtu au watu kuliko awapo peke yake; na kwamba, kicheko ni kitu kinachoambukiza.

## 1.4 Hitimisho kuhusu Mwingiliano wa Istilahi na Matokeo ya Ufutuhi

Maelezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu dhana mbalimbali zinazohusiana na futuhi yanaonesha kuwa, maana na misingi yake inakaribiana, kuingiliana, na kukamilishana kwa kiasi kikubwa. Dhana zote huwa na uwezo wa kusababisha kicheko, hali ya furaha, au ucheshi. Matokeo haya yanaweza kuwa ya wazi au fiche. Kwa msingi huo, makala haya hayajaziwekea mipaka dhana hizo; kwa pamoja, zimechukuliwa kama vijenzi tu vya ufutuhi.

Suala jingine la muhimu kumakinikiwa tunapovifikiria vijenzi na matokeo ya vijenzi hivyo linahusu uwezo wa kupatwa na ufutuhi. Jambo hili hutokea kwa viwango tofauti miongoni mwa watu. Ingawa ufutuhi ni dhana ya kiulimwengu (iko kwa watu wa jamii zote), lakini hii haimaanishi kuwa watu wote huwa na uwezo sawa wa kuunda au kuupokea. Hii ni kwa sababu jamii mbalimbali hapa

ulimwenguni hupishana katika vipengele vya maadili, itikeli, maarifa, na ujumi. Zaidi ya hivyo, tofauti za upokezi wao husababishwa na vigezo au sababu za kihistoria, kitamaduni, kisaikolojia, na kiepistemolojia. Akisisitiza kuhusu hoja hii, Ross (1998: 4) ambaye anajiegemeza katika dhana za utani na ucheshi anasema kuwa suala la kuwa na kionjo binafsi (cha kimaarifa na kisemantiki) ni la muhimu sana katika (uibuaji wa) ucheshi. Pia, kionjo cha mtu hubadilika kulingana na wakati na muktadha. Hii inamaanisha kuwa ni vigumu kwa watu wawili au zaidi kufanana katika jinsi ya kuutathmini utani.

Mpaka sasa mahitimisho ya kinadharia yanapwaya katika kutoa fasili na mipaka kuhusu dhana hizo. Kwa hiyo basi, wasomaji hupata mkanganyiko katika kutofautisha dhana za ucheshi, kicheko, kijembe, kejeli, matendo ya makusudi yazuayo kicheko, furaha au ucheshi, au yale yasiyo ya makusudi. Akizungumzia kuhusu tandabelua hii, Provine (2000) ananukuliwa na Billig (2005: 3) akisema:

> *...there has been too much speculation and insufficient experimentation on the area of humour. Much of the literature about laughter is still mired in its prescientific phase where anecdote, not empirical data, reign.*
>
> ...kumekuwapo na kudhani kwingi na majaribio yasiyotosheleza kuhusu uga wa ucheshi. Maandiko mengi kuhusu kicheko bado yangali katika hatua ya awali isiyo ya kisayansi ambapo taarifa za juujuu, zisizothibitishwa kisayansi, ndizo zinazoshamiri (tafsiri yetu).

Hapa, Provine anarejelea suala hili la mwingiliano wa fikra za baadhi ya wataalamu kuhusu kicheko na ucheshi.

Kwa upande wa matokeo yaletwayo na vijenzi vya ufutuhi, dhana ża kicheko na ucheshi huleta mkanganyiko mkubwa katika kuzielezea au namna ya kuzichukulia. Mathalani, mkanganyiko huu unaweza kuonekana hata katika nukuu ya Provine iliyotolewa hapo juu; ambapo, maelezo anayoyatoa hayaelekei kuwa na mwegamo wa moja kwa moja katika ama kicheko au ucheshi. Kimsingi, kuna jinsi ambavyo dhana hizi zinaingiliana.

Mnamo karne ya 18 na kurudi nyuma wataalamu wa zama hizo waliweka mipaka ya ucheshi kwa kuzingatia asili yake; yaani, ama ulitokana na uneni au matendo. Tabia iliyooneshwa na matendo ndiyo ilielekezwa zaidi katika dhana ya ucheshi; ilhali, ile iliyooneshwa na maneno ilielekezwa zaidi kwenye kicheko (Billig, 2005: 62). Kadiri siku na zama zilivyosonga mbele, maana ya dhana ya ucheshi imekuwa ikibadilika. Hivi sasa, dhana ya ucheshi inatazamwa na kuchukuliwa tofauti na ilivyokuwa inatazamwa takriban miaka 200 iliyopita. Kwa sasa, ucheshi ni dhana pana inayojumuisha vipengele na mazingira mbalimbali

yanayoonwa kuwa yanasababisha watu wacheke. Zaidi, mwondoko huo mpya wa jinsi ya kuuchukulia ucheshi umezidisha pia mshonano wa vipengele, na hivyo, kusababisha utata zaidi katika kuusoma na kuuelezea.

Hivyo basi, ili kurahisisha uelewa wa dhana mbalimbali zinazobebwa na kicheko, uchangamfu, ucheshi, na furaha, ni vyema dhana kuu ya ufutuhi itumike. Aidha, umuhimu wa kutumia dhana hii ya ufutuhi unatokana na mwingiliano mkubwa wa kimaana na kidhima uliopo baina ya vijenzi mbalimbali vya ufutuhi. Hoja hii inamaanisha kwamba makala haya yametumia dhana ya ufutuhi kwa kuamini kwamba, kwayo, dhana nyinginezo za utani, ubeuzi, kejeli, dhihaka na vijembe zitakuwa zimeshughulikiwa kwa pamoja. Kwa upande mwingine, matumizi ya dhana hii yanaakisi kasi na kani za mwondoko wa kiwakati.

Zaidi, wazo la kuitumia dhana ya ufutuhi, Chambilecho Rocha Chimerah[4], ni sawa na kurudi katika asili kuhusu suala zima la matumizi ya lugha. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, kwa kawaida, binadamu alengapo kuzungumzia suala linalohusiana na ufutuhi (ama vijenzi au matokeo yake) hufanya hivyo kwa kurejelea dhana za jumla, na siyo mahususi. Chimerah anasema:

> ...hivyo vyote (vijenzi vya ufutuhi) huwa havibaguliwi katika matumizi ya lugha. Katika fasihi, huwa tunavitenga na kuvibagua. Kwa mfano, tutazamapo filamu au tamthiliya ikiigizwa jukwaani, ni vigumu sana kusema 'sasa hapo ni kejeli' au 'hilo sasa ni fumbo' n.k. Hizi ni mbinu zinazopatikana katika lugha kulingana na tamaduni zao. Zote huwapeleka watu katika kucheka au kufurahi. Wanafasihi tumezipa majina hayo ili tuweze kuzielewa kwa urahisi zaidi. Hivyo, wazo la kuvijumuisha vipengele hivyo kimatumizi kupitia hiyo istilahi ya ufutuhi ni sahihi. Yaani, hiyo ni sawasawa na kurudi katika asili ya matumizi sahihi ya lugha.

Licha ya fikra hizi za Chimerah, ukweli mwingine unaoshadidia usahihi na ufaafu wa kutumiwa kwa dhana ya ufutuhi ni ugumu wa kupatikana kwa maelezo ya kinadharia kuhusu vijenzi vya ufutuhi vichukuliwapo kwa namna ya upweke-pweke. Fasili, mijadala, na nadharia zinazofafanua kila kijenzi au matokeo ya ufutuhi kwa namna ya upweke hukosa utoshelevu kutokana na mwingiliano mkubwa wa kimaana na kimatumizi baina ya dhana, hali, au matokeo hayo. Mathalani, ni kawaida kumsikia mtu akimkejeli au kumtweza mwenzake, na baadaye akahitimisha kwa kusema '...nilikuwa nakutania tu.' Hapa, yawezekana mtu huyo alimfumba, alimkejeli, alimng'ong'a, au alimtweza; pamoja na hivyo, ni vigumu kwa mtu huyu kusema 'nilikuwa nakutweza tu' au 'nilikuwa nakufumba tu.'

Maelezo yote hayo, hatimaye, yanatuleta katika hoja ya kupanua mawanda ya kushughulikia masuala yahusianayo na raha, furaha, kicheko, na ucheshi kwa

---

[4] Mazungumzo binafsi baina ya Rocha Chimerah na mwandishi yaliyofanyika Agosti 28, 2013 jijini Nairobi. Chimerah ni Mhadhiri Mwandamizi wa Fasihi katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki kilichomo jijini humo.

kutumia istilahi ya ufutuhi. Kwa hiyo basi, ufutuhi, katika makala haya, unajadiliwa kama dhana yenye sifa zifuatazo:

a) Ni dhana jumuishi ambayo hufumbata vijenzi mbalimbali vyenye uwezo wa kutoa matokeo yanayolandana;
b) Ni wa mwanadamu, yaani, huundwa, hutolewa, na huelekezwa kwa mwanadamu; vilevile, ni kwa ajili ya mwanadamu;
c) Mpokezi wa hali au matendo ya kifutuhi hupatwa na ufutuhi kufuatia kuwapo kwa dhana ya 'kusahau'. Hii ni hali ya kutokuwa na fikra za masuala mengine yanayoumiza au kusongamana akilini. Kwa wakati huo, hali hiyo ya 'kusahau' hutokea kwa muda;
d) Huweza kudhihirishwa kwa kutumia maumbo mbalimbali kama vile maneno ya mdomo, maandishi, matendo, michoro ya vibonzo au picha tuli (ufutuhi wa maneno ya ana kwa ana, na ule wa utendaji una historia ndefu sana. Ufutuhi wa maandishi na wa uchoraji ulifuatia baadaye);
e) Si suala la kinasibu, bali ni la kikanuni, na;
f) Ni dhana inayoambukiza. Hoja hii inamaanisha ukweli ufuatao: mosi, ufutuhi ni jambo litokealo katika mazingira ya kuwapo kwa watu wengi kuliko mazingira ya upweke. Pili, kuna uhusiano wa karibu sana baina ya ufutuhi na misingi ya nadharia za kipokezi. Tatu, (hoja hii yahusiana na hoja ya pili), mtu akitaka kuusoma na kuuelewa ufutuhi kwa misingi ya utendekaji au kitaaluma, basi yafaa ajielekeze katika kuwachunguza wengine kuliko kujichunguza yeye mwenyewe.

## 2.0 Kutoka Futuhi hadi Ufutuhi

Kusudio la sehemu hii ni kuonesha uhusiano wa futuhi na ufutuhi. Kama ilivyokwishadokezwa hapo juu, msingi wa futuhi umo katika tamthiliya. Hivyo, toka zama za Wayunani wa kale, futuhi ziliifikia hadhira kupitia jukwaa. Baadaye, futuhi ziliingizwa pia katika ushairi (ambao Aristotle, katika *The Poetics*, anauita 'ushairi uliopindishwa'). Hivyo, hadi kufikia hatua hii, tayari futuhi ilikwishaanza kupoteza uasili wake. Kadiri zama zilivyokuwa zinasonga mbele, ndivyo wasanii walivyoongeza fikra za kuipanua futuhi kwa kuiingiza katika sanaa tofautitofauti kama vile muziki, uchongaji, uchoraji, na ufumaji. Upanuzi huu ulijumuisha pia vipengele vya maudhui, muundo, pamoja na mtindo. Ni katika zama hizi za kuipanua futuhi katika sanaa za namna tofauti ndipo pia msisitizo wa kiufafanuzi ulianza kuchukua mkondo mpya wa kuzitofautisha dhana za futuhi (*comedy*), –a futuhi (*comedic*), na ufutuhi (*comic*). Licha ya kumaanisha hali au mazingira ya furaha, ucheshi na kicheko, dhana ya *comic* pia hutumiwa katika marejeleo mbalimbali kumaanisha '–a futuhi' na/au '–a kifutuhi.'

Chimbuko la matumizi ya dhana ya ufutuhi limo katika fikra za tapo la Urasimi Mpya ambalo kwa mujibu wa Senkoro (1987) lilishika hatamu kuanzia

mwishoni mwa karne ya 17 (miaka ya 1680 - 1780 BK). Harakati za awali za kuipanua futuhi na kuiingiza katika sanaa nyinginezo zilishuhudia fikra za wasanii zikiielekeza katika uchoraji. Katika kuelezea hali mbalimbali zilizonasibishwa na futuhi katika michoro, ndipo dhana hii ya ufutuhi ilipoanza kushuhudiwa ikitumiwa. Katika kipindi hicho kulikuwa na dhana kama vile '*colour comic*' ('ufutuhi wa rangi') na '*comedy of colour*' ('futuhi ya rangi'). Baadaye, ndipo dhana hii ya ufutuhi ikaanza kutumiwa pia katika magazeti, majarida, na katika fasihi andishi kwa ujumla, hususan, katika utanzu wa riwaya (Bergengen, 2004: 90). Mathalani, katika karne ya 18 ambayo hujulikana pia kuwa ni zama za mwana-tashtiti maarufu Jonathan Swift[5], dunia ilishuhudia akichapisha riwaya yake maarufu ya *Gulliver's Travels* (1726).

Vuguvugu la kuibuka kwa ufutuhi wa kisasa (hali iliyopo sasa) ambapo takriban nyanja zote muhimu za maisha ya mwanadamu zinaendeshwa kwa kunyunyiziwa ufutuhi, lilianza katikati ya karne ya 18. Billig (2005: 12) anafafanua kuwa mnamo miaka ya 1840 hadi 1870 ilizuka dhana ya 'dunia ya ki-ucheshi'. Hiki kilikuwa kipindi ambacho 'haiba na hadhi ya ki-ucheshi' ilianza kutambuliwa na kusambaa ulimwenguni. Fikra hizi mpya kuhusu jinsi ya kuuchukulia ucheshi zilibadili pia mtazamo wa awali wa jinsi ya kumchukulia mwanadamu kwa jumla. Uwezo wa kuzua ucheshi, katika kipindi hiki, ulichukuliwa kama kionjo maalumu cha kibinafsi ambacho hakiwezi kuwa kwa kila mtu. Hivyo, mwanadamu alianza kutazamwa na kuthaminiwa kama kiumbe binafsi mwenye karama tofautitofauti (ikiwamo ya kuzua masuala mbalimbali ya ufutuhi kama vile ucheshi).

Katikati ya karne ya 20 yalishuhudiwa mabadiliko mengine kuhusiana na hadhi ya ufutuhi ambapo ufutuhi ulichukuliwa pia kama mkakati wa kuubadili au kuuondoa uandishi na usomaji wa kikanuni au usomaji wa kirasimi. Mnamo mwaka 1954, huko Marekani ilianzishwa Mamlaka ya Sheria za Ufutuhi (*Comics Code Authority*). Chombo hiki kilikuwa na dhima muhimu ya kuratibu na kusimamia ufundishaji, utungaji, uchapishaji, usambazaji, na usomaji au utazamaji wa kazi mbalimbali za kifutuhi. Lengo hapa lilikuwa ni kuwahamasisha watu ili waongezeke katika kuziandaa na kuzipokea kazi za kifutuhi. Vilevile, shabaha nyingine ilielekezwa katika kudhibiti suala la kupotoka kwa maadili na itikeli za kijamii kupitia ufutuhi. Matunda ya chombo hiki yalianza kuonekana miaka ya 1970 ambapo watu wenye vionjo vya kifutuhi waliokuwa wanafanya shughuli zao chini kwa chini wakaanza kujitokeza hadharani. Kukawa na mfumuko wa uchapishaji wa kazi nyingi za kifutuhi. Hata hivyo, bado kazi hizo zilitolewa kwa kuzingatia mitindo binafsi.

---

[5] Jonathan Swift ni mwanafasihi maarufu raia wa Ireland aliyeishi baina ya Novemba 30, 1667 na Oktoba 19, 1745. Huyu anachukuliwa kuwa ni miongoni mwa wataalamu wa mwanzo kusana nathari andishi zenye ufutuhi kupitia nyenzo ya tashtiti. *Gulliver's Travels* ni andiko-bora lake lililopata mashiko ulimwenguni kote (*Encarta*, 2007).

Mnamo miaka ya 1980 na 1990 iliibuka dhana ya futuhi nzito au futuhi tata. Hii ilijumuisha utata au uchangamani katika vipengele kama vile vya wahusika (na uhusika wao), na msuko wa migogoro au matukio. Wimbi hili jipya lilifanikiwa kuutikisa na kuubadili mwelekeo wa uandaaji na upokezi wa kazi za kifutuhi katika maeneo tofauti ya sanaa kama vile fasihi (ukiwemo utanzu wa riwaya), filamu, na uchoraji. Pamoja na hayo, kumekuwa na tofauti katika uundwaji au utokeaji wake miongoni mwa kazi za kuonwa, kusomwa, kusikika, au kuonwa na kusikika (Aldama, 2009: 4-5).

Harakati zilizobainishwa hapo juu (za kushadidia kuwapo kwa dhana ya 'dunia ya ki-ucheshi', kutambuliwa kwa 'haiba na hadhi ya ki-ucheshi', pamoja na uanzishwaji wa vyombo vya kusimamia na kuongoza masuala ya ufutuhi kama 'Mamlaka ya Sheria za Ufutuhi') zilisaidia kwa kiasi kikubwa kusambaza fikra za ufutuhi ulimwenguni. Hatimaye, kutokana na harakati hizo, jamii mbalimbali duniani ziliingia katika karne ya 21 zikiwa zimeongeza matumizi ya ufutuhi kama nyenzo ya kuendeshea maisha yao katika nyanja kama vile za siasa, mfumo wa uhabarishaji, uelimishaji, pamoja na michezo.

Hivi sasa, takriban kila chombo cha habari (runinga, magazeti, na redio) nchini Tanzania kina programu ya ufutuhi. Mathalani, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1) hurusha vipindi viwili; cha kwanza ni kile cha '*Ze Orijino Komedi*' kwa muda wa dakika 60. Kingine ni kile cha '*Fataki*' ambacho huhusisha uwasilishaji wa ushairi wenye vipashio vingi vya ufutuhi. Kituo cha EATV kinarusha kipindi cha '*Ze Comedy Show*'. Pia kituo cha ITV hurusha kipindi cha '*Mizengwe*' kwa muda usiopungua dakika 30. Kwa upande wa kituo cha *Star* TV, kuna vipindi viwili vinavyorushwa kwa muda wa dakika 60 kila kimoja. Vipindi hivyo ni '*Futuhi*' na '*Vunja Mbavu*.' Kwa upande wake, kituo cha *Channel Ten* hurusha kipindi cha '*Vimbwanga Time*' na '*Kanjanja Time*' kwa muda wa zaidi ya dakika 60. Hii inamaanisha kwamba hadhira ya vituo hivyo vya runinga huwa inapata muda wa kutosha kufuatilia vipindi vya ufutuhi.

Zaidi ya vipindi hivyo vya ufutuhi wa moja kwa moja, hivi sasa umefanyika upanuzi kwa kuuingiza ufutuhi hata katika programu ambazo awali zilionekana ni za ki-dhati. Programu za taarifa za habari katika baadhi ya vituo vya runinga pia huchanganywa na vipande vyenye ufutuhi. Mathalani, taarifa za habari za ITV, na *Star* TV hujumuisha vipengele vya vibonzo. Hali hii ya kushamiri kwa matumizi ya ufutuhi inashuhudiwa pia katika upande wa vituo vya redio. Huku nako, licha ya kuwapo kwa programu za moja kwa moja za ufutuhi, kuna mwondoko mpya wa matumizi ya vionjo vya kifutuhi katika utangazaji wenyewe. Kumekuwa na ushindani miongoni mwa watangazaji katika kutumia vionjo vyenye ufutuhi wakati wa kutangaza vipindi vyao. Kwa maoni ya mwandishi, wamiliki au watangazaji hao hufanya hivyo ili kuivutia na kuivuta hadhira. Na kwa baadhi ya vituo, yumkini, suala hili laonekana kuwa ni sera au mwelekeo wao wa jumla.

Hali iko hivyo pia katika majarida na magazeti nchini Tanzania. Katika upande huu, ufutuhi hudhihirishwa kupitia maneno, vibonzo, pamoja na picha tuli. Hali hii, chambilecho Senkoro (2004), ilichipuka na kushamiri wakati wa uanzishaji wa mfumo wa vyama vingi vya siasa katika miaka ya mwishoni mwa 1980 na ile ya 1990. Kuanzia kipindi hiki, tasnia ya habari za magazeti imekuwa ikitumia sana vibonzo katika kuwasilisha mambo mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na yale ya kijamii. Kutokana na kasi kubwa ya kukubalika na kupendwa kwa magazeti na majarida yaliyokuwa na mwelekeo wa kifutuhi, idadi yake ikaongezeka. Mifano ya majarida yaliyoshika hatamu wakati huo ni *Sani* na *Bongo*. Kwa upande wa magazeti, mifano yake ni *Sanifu, Komesha, Kasheshe*, na *Acha Umbea*. Maudhui ya magazeti haya yalizungumzia mambo mbalimbali yaliyoihusu jamii kwa mbinu ya kifutuhi. Licha ya magazeti hayo ambayo huonwa kuwa ni ya kifutuhi, hata magazeti yaonwayo kuwa ni ya dhati yamekumbwa na mkondo huu. Mfano mmojawapo wa magazeti-dhati hayo ni *Majira* ambalo hutolewa kila siku na kuchapisha kibonzo cha 'Kingo' ambacho huwa hakitumii maneno. Gazeti jingine la kila siku la *Nipashe* litoalo kibonzo cha 'Kabwela'. Pia, katika gazeti la *Lete Raha* kuna vipengele vya 'Vituko Uswahilini', pamoja na vibonzo vya 'Cheka Kispoti' na 'Gwiji'. Gazeti la *Mwananchi* hutoa vibonzo vya 'Masoud' na 'Bwana Chezo.' Gazeti la *Mtanzania* hutoa kibonzo cha 'Zero. Aidha, kuna magazeti maalumu ya habari za michezo ambayo hutoa ufutuhi kwa maandishi, vibonzo au picha. Kwa mfano, kuna gazeti la *Champion* ambalo hutoa vibonzo vya 'Chizika na Soka' na 'Bongo Spoti.' kuna gazeti jingine la *Mwanaspoti* lichapishalo vibonzo vya 'Kipute,' 'Vijimambo,' na 'Kijiweni Wikiendi.'

Kwa ujumla, hii ni ithibati nyingine muhimu ya kwamba, kwa sasa, pengo lililokuwapo wakati wa Zama za U-Aristo-Plato[6] na zama za sasa kuhusu fikra za u-futuhi na udhati limepungua au kufutika kabisa. Kwa sasa, kuna ufungamano mkubwa baina yazo.

## 3.0 Nadharia za Ufutuhi

Maelezo ya hapo juu yamedokeza kwamba msingi mkubwa wa ufutuhi ni kutokea kwa ucheshi, kicheko, na furaha kupitia vijenzi mbalimbali (kimoja kimoja au vikiungana baadhi yavyo). Shabaha kuu ya sehemu hii ni kutoa ufafanuzi kuhusu utokeaji wake. Kuna nadharia kuu tatu zinazoelezea masuala haya ya kicheko, furaha, na ucheshi. Nazo ni Nadharia ya Mkwezo, Nadharia ya Msigano, na Nadharia ya Burudiko.

---

[6] Dhana hii imetumiwa kama kisawe cha dhana ya Kiingereza 'Aristo-Platonic Era'; yaani, kipindi cha Urasimi ambacho kilitawaliwa na fikra za wataalamu wawili wa Kiyunani — Aristotle na Plato.

### 3.1 Nadharia ya Mkwezo

Kwa mujibu wa Billig (2005), chimbuko la nadharia hii ni falsafa za Uyunani ya kale. Waasisi wake ni Plato na Aristotle. Hata hivyo, wao hawakuitazama dhana hii kwa jicho la kinadharia, bali waliitazama kama dhana tu iliyokuwa inajitokeza katika ufafanuzi wa masuala mbalimbali. Plato, kwa mfano, katika kazi yake ya *The Republic*, anasema: "*we laugh at inferior or ugly individuals because we feel a joy at feeling superior to them.*" Yaani, tunawacheka watu wenye uduni au wenye sura mbaya kwa sababu twajisikia furaha kujiona tuna hadhi kuliko wao.

Dhana ya ufutuhi ilianza kutazamwa kwa jicho la kinadharia mnamo karne ya kumi na saba (17). Mtaalamu anayeheshimika kama mtu wa kwanza kuitazama hivyo ni Thomas Hobbe[7]. Katika karne hiyo juhudi za Hobbe zilionekana kupitia maelezo ya kisayansi aliyoyatoa kuhusu vipengele vya ufutuhi. Maelezo yake kuhusu sababu za kutokea kwa kicheko na ucheshi yalionekana kuwa na mashiko kuliko maelezo ya awali. Kwa jumla, nadharia hii inadai kuwa mtu hucheka kwa sababu ya kujiona kuwa yuko katika hadhi ya juu; na kwamba, wakati huo mtu hujikweza na kujiweka huru zaidi akiwa amejitenga na hali yoyote ya uduni. Kutokana na msingi huo, nadharia hii hujulikana pia kama 'Nadharia ya Ugandamizaji.' Kucheka hapa kunanasibishwa moja kwa moja na kutosheka au kuridhika kwa nafsi ambako, aghalabu, huzaa furaha. Yaani, mtu anapocheka, hutawaliwa na raha ya aina fulani na kujiona yuko katika tabaka la pekee hata kama anazungukwa na matatizo. Punde atokapo nje ya muktadha wa kicheko chake ndipo huweza kurudi katika kuyawazia matatizo yake. Nadharia hii ya Mkwezo, kwa mujibu wa Provine (2000) na Morreall (1983) ambao wamenukuliwa na Billig (2005), ilidumu kwa takriban miaka elfu mbili kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Nadharia ya Msigano.

### 3.2 Nadharia ya Msigano

Nadharia hii inashikilia ukweli kuwa kicheko hutokea kwa mtu mara tu mawazo yake yanapokataa kuafiki neno au jambo lililotendwa baada ya kubaini kuwa liko kinyume au tofauti na lilivyopaswa kuwa. Hivyo, madai ya msingi hapa ni kubainika kwa msigano baina ya neno au jambo lilivyo na jinsi lilivyopaswa kuwa. Sehemu kubwa ya wataalamu waliojihusisha na nadharia hii ni wale watokao katika ukanda wa Uingereza, Wales na Uskochi. Nao ni kama vile Lord Kames, Dugald Stewart, David Hartley, na Francis Hutcheson. Wengine watokao nje ya

---

[7] Thomas Hobbes ni mwanafalsafa na mwananadharia wa Kiingereza aliyeishi miaka ya 1588-1679. Pamoja na kuwa aling'ara sana katika nyuga za siasa na falsafa, mtaalamu huyu pia alifanya mengi ya kukumbukwa katika uga wa fasihi. Fikra zake zilizomtangaza katika fasihi zilianzia katika siasa. Huko, alikuwa mtetezi sana wa dhana yake ya '*Political Absolutism*'; yaani, 'utamalaki wa kisiasa' aliyoitoa kupitia chapisho lake *Leviathan* (1651). Ni katika chapisho hilohilo pia kunapatikana mawazo yake kuhusu dhana ya ufutuhi.

ukanda huo ni Arthur Schopenhauer, Herbert Spencer, Sigmund Freud na Emmanuel Kant (Schuette, 2010). Kushamiri kwa mikondo ya kitaaluma iliyozaliwa katika maeneo haya ya Uingereza na nchi-viambata vyake kulichochewa sana na kusainiwa kwa waraka wa Muungano baina ya nchi hizo mnamo mwaka 1707 (Schuette, 2010; Billig, 2005). Miongoni mwa wataalamu hao, Francis Hutcheson ndiye anajitokeza kuwa kinara zaidi katika kuipaza nadharia hii. Huyu, kupitia kitabu chake kiitwacho *Thoughts on Laughter* kilichochapishwa mwaka 1725, alisisitiza kuwa msigano ndicho kiini cha kutokea kwa ufutuhi.

Mkondo huu mpya wa fikra kuhusu jinsi ya kuyachukulia masuala yahusianayo na kicheko na ucheshi uliibuka na kushamiri mnamo karne ya 18. Shabaha yake kuu ilikuwa kuzihakiki na kuzipinga fikra za John Hobbes kuhusu kicheko na ucheshi. Wakati fikra za ucheshi na kicheko katika mkondo wa awali (ule wa Nadharia ya Mkwezo) zilielekezwa kwenye vionjo vya mtu akumbwaye na kicheko na ucheshi, fikra za nadharia hii zilielekezwa katika vionjo vya unyume vinavyohusiana na matukio au uneni au hali zizuazo ucheshi na kicheko. Hapa, uchunguzi wa fikra za ucheshi na kicheko hasa zilihusishwa sana na miktadha ya siasa, ujumi, maadili, na itikeli za jamii na asasi mbalimbali. Katika miaka ya mwanzo ya kuzaliwa kwa Nadharia hii ya Msigano, wataalamu walibishana na kupishana kuhusu istilahi iliyofaa kutumiwa kama jina la nadharia. Kwa mujibu wa Tave (1960) ambaye amenukuliwa na Billig (2005: 64), dhana ya *Incongruity* ilitumiwa kwa mara ya kwanza katika maandishi na Mark Akenside kupitia kitabu chake kiitwacho *The Pleasure of Imagination* (1744).

Kwa ujumla, nadharia hii inasisitiza kuwa, kimuundo, dhana au hali yoyote yenye uwezo wa kuzua ufutuhi lazima iwe na pande mbili zinazosigana 'kwa undani' (kulingana na tafsiri au uelewa wa mpokeaji). Utokeaji wa ufutuhi kwa misingi ya nadharia hii hujikita katika utofautishaji wa dhana au hali ambazo zinaonekana kulandana kwa sura au mwonekano wa jumla; lakini, kwa undani huwa tofauti. Katika hatua ya awali, dhana hizo hukusanywa kwa pamoja katika fikra za mpokeaji. Kitendo hiki hufanywa au hutokea kwa haraka sana. Kisha, kwa kutumia misingi ya tajiriba kuhusu hali au dhana hizo, mpokeaji huzizamia na kubaini kutofautiana kwazo; hatimaye hujiwa na ufutuhi. Utendekaji wa michakato yote hii huhitaji misingi ya kisaikolojia, kihistoria, na ya kiutambuzi.

## 3.3 Nadharia ya Burudiko

Maswali ya kitafiti kuhusu namna gani na wakati gani kicheko na ucheshi hutokea yaliendelea kusumbua fikra za wataalamu mbalimbali na kuibua Nadharia ya Burudiko mnamo nusu ya pili ya karne ya 19. Waasisi wake ni Waingereza wawili, Alexander Bain (1818-1903) na Herbert Spencer (1820-1903). Hawa waliyahusisha na kuyaendeleza mawazo ambayo yalichimbuliwa na watangulizi wao kama vile Ben Johnson (1572-1637) na John Locke (1632-1704). Kiini cha fikra za nadharia hii kilichimbuliwa na hamu ya kutaka kujua jinsi akili ya

mwanadamu inavyochakata mambo kwa msingi wa kifiziolojia. Hiki ni kipindi ambacho kilitamalakiwa na fikra za kuichambua akili ya mwanadamu kwa mwegamo huo. Mwaka 1859 Bain alichapisha kitabu cha *The Emotion and the Will* ambapo maudhui yake yalijiegemeza moja kwa moja katika dhana hiyo. Mwaka mmoja baadaye, 1860, Spencer alitoa maoni makali ya kihakiki kuhusu maudhui hayo. Izingatiwe pia kuwa mwaka 1859 ilishuhudiwa kuchapishwa kwa kitabu maarufu cha Charles Robert Darwin (1809-1892) kiitwacho *On the Origin of Species*; na baadaye akachapisha *The Expression of the Emotions in Man and Animals* (1872). Majibizano ya wataalamu hawa yalitoa mchango mkubwa katika kuzaliwa kwa mawazo ya nadharia hii yaliyoelekezwa katika namna gani mifumo ya neva pamoja na ule wa akili ihusikavyo na upitishwaji wa kemikali mbaya za mwilini (Billig, 2005: 86-87).

Kwa ujumla, Nadharia ya Burudiko, kama ilivyofafanuliwa na wataalamu hao, inachukulia kicheko kama burudani itoayo tiba kwa aina mbalimbali za maradhi. Hii ni kwa sababu kicheko hubeba dhima ya kusukuma msongamano wa mawazo kutoka akilini na mwilini mwa mtu. Majumuisho haya yametoka katika fikra za Ben Johnson ambaye mnamo karne ya 16 aliasisi 'Mkabala wa Vimiminika Vinne vya Mwili.' Alifanya hivyo kupitia kazi zake maarufu za kifutuhi za *Every Man in His Humour* (1598) na *Every Man Out of His Humour* (1599). Mkabala huu unasisitiza umuhimu wa kuwapo kwa uwiano mzuri baina ya vimiminika muhimu vinne vya mwili ambavyo ni damu, nyongo nyeusi, nyongo ya njano, na uteute. Vimiminika hivi huufanya mwili pamoja na akili kuwa na afya njema, hivyo, kuuwezesha kufanya kazi zake zote kwa urahisi na ufanisi. Lakini kukiwa hakuna uwiano mzuri baina ya vimiminika hivyo, damu ambayo ndiyo imetamalaki mwilini kuliko hivyo vingine husababisha msongo wa mambo, hatimaye hasira. Kwa ufupi, hali za raha, furaha, au kicheko ni matokeo ya utendekaji wa michakato ya uwianishaji wa vimiminika hivyo kwa kiasi cha kutosha; na kwa upande mwingine, hali za maumivu, jitimai na namna nyinginezo za kitanzia ni matokeo ya utendekaji hafifu wa michakato ya uwianishaji wa vimiminika hivyo. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Johnson, wazo la kuzuia matatizo hayo ndilo hasa lililosababisha kuwapo kwa futuhi, na baadaye, ufutuhi.

### 3.4 Hitimisho kuhusu Nadharia za Ufutuhi

Maelezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu nadharia tatu za ufutuhi yanatuangazia mambo muhimu yafuatayo: mosi, inaonekana kuwa kuna muumano mzuri baina ya mabadiliko ya hali za kijamii hapa ulimwenguni na kuzuka kwa nadharia za ufutuhi. Mathalani, kutokana na ukweli kuwa wakati wa urasimi binadamu alitawaliwa na hali ya kuthamini na kuzingatia maadili na thamani ya mtu (kutokana na ama kuwa tajiri au mtu wa kutoka katika nasaba bora au maskini au mtu wa kutoka katika nasaba duni), ikazuka dhana ya kujikweza; na hatimaye,

kuibuka kwa Nadharia ya Mkwezo. Kisha, ikaja Nadharia ya Msigano. Yumkini, wakati huu kulikuwa na vuguvugu la namna mpya ya kufikiri na kutathmini kuhusu mifumo mbalimbali ya maisha kutokana na tukio la mapinduzi ya viwanda. Fikra za umuhimu wa binadamu kuwa na 'burudani' zilichipuka kadiri dunia ilivyoendelea kubadilika na kuingiliana katika vipengele vya kijamii na kiuchumi, ugumu wa maisha uliongezeka. Ugumu huo wa maisha nao ukaongeza misongo, na misawijiko ya kimaisha miongoni mwa wanajamii. Kutokana na kushamiri kwa misawajiko hiyo ya kimaisha ambayo husababisha athari za kiafya na kijamii kwa wanajamii, ndipo jamii ikalazimika kutafuta namna ya kuipunguza. Yumkini, harakati hizo zina mchango mkubwa katika kuibua fikra za Nadharia ya Burudiko. Zama hizo ndizo hizi zinazoendelea hadi sasa ambapo matumizi ya ufutuhi kama kiburudisho na nyenzo ya kushusha misawajiko ya wanajamii yameshika hatamu.

Pili, nadharia hizo zinatupambanulia mitazamo mikubwa miwili inayoelezea jinsi mtu anavyoweza kupatwa na ufutuhi (na hivyo kuweza kuudhihirisha). Mtazamo wa kwanza ni ule usemao kuwa ufutuhi hutokana na kuridhika kwa nafsi; kwamba, ni mdhihirisho wa jinsi mtu alivyopendezwa na vionjo alivyoviona au kuvisikia. Mtazamo wa pili unashikilia kuwa ufutuhi hutokana na aina fulani ya ubezaji, upingaji, uhojaji, au uhakiki kutokana na mtu kukumbwa na hali ya kutokukubaliana katika jambo, hali, kitu au tendo fulani. Ijapokuwa tukio hili hutokea kwa haraka, huhitaji na hutegemea sana misingi ya kiutambuzi na tajiriba. Misingi hiyo ndiyo imsaidiayo mtu kupata hisia za kugongana au kupishana kwa fikra baina ya uhalisi wa uelewa wake kuhusu jambo husika dhidi ya kile kilichodhihirishwa mbele yake kuhusiana na jambo hilohilo (Kennedy na Gioia, 2007).

Tatu, maelezo hayo ya kinadharia yanatubainishia kuingiliana na kutofautiana kwa matokeo ya ufutuhi ambayo ni ucheshi, kicheko na furaha. Kuhusu hali ya kuingiliana kwayo, kwa jumla, haya yote hutokana na vijenzi vilivyoainishwa katika sehemu za hapo juu. Zaidi, huingiliana kwa namna ya kiukamilishano. Mathalani, kwa kiasi kikubwa, tabia ya ucheshi kwa mtu hudhihirishwa na hali ya furaha. Kwa upande mwingine, kuna tofauti kama ambavyo kila dhana imefafanuliwa.

## Marejeleo

Aristotle, (2002). *The Poetics*. Bernadete, S. na Da, M. (Wafasiri). South-Bend, Indiana: St. Augustine Press.

Aldama, F.L. (2009). *Your Brain on Latino Comics*. Austin: The University of Texas Press.

Attardo, S. (2001). *Humorous Texts: A Semantic and Pragmatic Analysis*. Berlin and New York: Mouton de Gruyter.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

Beck, R.M. (1999). Comic in Swahili or Swahili Comic? Swahili Forum, Vol. 60, pg. 67 – 101. AAP.

Bergengen, R. (2004). *Arguing Comics: Literary Masters on a Popular Medium*, Heer, J. na Worcester, K. (Wah.). Mississipi: University Press of Mississipi.

Billig, M. (2005). *Laughter and Ridicule: Towards a Social Critique of Humour.* London: Sage Publications.

Dauphin, V.P. (2007). Sarcasm in Relationships. *Journal of Pragmatics, 32* (2000) pg.1467-88. New York: Oxford University Press, Inc.

Diegner, L. (2002). Allegories in Euphrase Kezilahabi's Early Novels. *Swahili Forum*, Beck, R.M. et al. (Edts.), *Vol. 72*, pg. 43-74. AAP.

*Ensaiklopidia ya Encarta* (2007). Art and Literature. Microsoft Corporation.

Fry, W.F. (2000). Humor and Synergy. *Journal of Humor & Health Journal, Vol. 9* (3), pg. 1-3.

Fry, W.F., & Allen, M. (1998). *Creating Humor: Life Studies of Comedy Writers* (2nd Edition.). New Brunswick: Transaction Books.

Fry, W.F., & Allen, M. (1976). Humor as Creative Experience: The Development of a Hollywood Humorist. *Humor and Laughter: Theory, Research and Application*, A.J. Chapman & H.C. Foot (Eds.). London: John Wiley & Sons.

Fry, W. (1963). *Sweet Madness: A Study of Humor.* CA: Pacific Books, Palo Alto.

Green, E.J. (1977). *Menander to Marivaux: The History of the Comic Structure.* Alberta: The University of Alberta Press.

*Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010). Nairobi: Oxford University Press.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004). Nairobi: Oxford University Press.

Kennedy, X.J & Gioia, D. (2007). *Literature: An Introduction to Fiction, Poetry, Drama, and Writing* (Tenth Edt.). New York: Pearson – Longman.

Kezilahabi, E. (1976). 'Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya'. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

Mohamed, M. na Mohamed, S. (2004). *Kamusi ya Visawe.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mrikaria, S.E. (2010). Kejeli katika Fasihi. *Swahili Forum, Toleo la 17*, Beck, R.M. et al. (Wah.), uk. 104-125. AAP.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M.M. (1986). 'The Nanga Epos of the Bahaya: A Case Study in African Epic Characteristics,' A PhD Thesis, University of Dar es Salaam.

Olson, D.S. (2007). *Broken Laughter: Selected Fragments of Greek Comedy*. Oxford: Oxford University Press.

Provine, R.R. (2000). *Laughter: A Scientific Investigation*. London: Farber and Farber.

Ross, A. (1998). *The Language of Humor*. New York: Routiledge.

Schuette, C. (2010). Gelatology, the Study of Laughter. Iliyosomwa tarehe 06/05/2012 katika http://www.bellaonline.com/articles/art38021.asp

Sengo, T.S. & Lucas, S.A. (1975). *Utani na Jamii ya Wakwere*. Nairobi: Foundation Books Limited.

Senkoro, F.E.M.K (2004). Fools, Drunkards, and Imbeciles Tell More Truth: Whither Satire in Tanzania? *Jarida la Kiswahili, Juzuu ya 67*, Y.M. Kihore (Mh.), kur. 25-30. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Wamitila, K.W. (2003a). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K.W. (2003b). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Whipple, C. na Calvert, S. (2008). The Connection between Laughter, Humour, and Good Health. *Journal of Health Education through Extension Leadership*. Kentucky: Kentucky University Press.

Yahya-Othman, S. na wenzake (h.t), The Structure and Function of Jokes in Tanzania. Ripoti ya Utafiti Mdogo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.